



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI



Kumb.Na .HW/S.20/96/56

12/03/2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

1.0 UTANGULIZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni anawatangazia Wananchi wote Raia wa Tanzania wenye sifa zinazohitajika kuomba kujaza nafasi wazi baada ya kupokea kibali cha ajira mbadala chenye **Kumb Na. FA.228/613/01/059** cha tarehe **11 Desemba, 2023** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

1.1 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 1)

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea.
- Astashahada/Cheti NTA/LEVEL 5 katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii au Sayansi ya Jamii kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali .

1.3 KAZI NA MAJUKUMU

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao kuwa mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utelekezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kijiji
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuondoa njaa umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji
- Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika Kijiji
- Kupokea kusikiliza na kutatua malalamiko ya migogoro ya Wananchi
- Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kazi

1.4 MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya mshahara ya Serikali ngazi ya Mshahara itakuwa TGS B

2.0 MAELEZO/ MASHARTI YA JUMLA

i) Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri si zaidi ya miaka 45 na sio pungufu ya Miaka 18.

ii) Waombaji wenye ulemavu wnahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira aina ya ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

iii) Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza **Curriculum Vitae (CV)** yenye Anwani inayotumika, namba ya simu na **Anuani ya barua pepe (E-mail address)** pamoja na majina ya Wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.

iv) Matokeo ya muda (**Provisional/Testimonials/Statement of results**) havitakubaliwa.

v) Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.

vi) Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokua kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

vii) Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishie barua zao za maombi ya nafasi ya kazi kwa waajiri wao na waajiri wao wajiridhishe iapasavyo.

viii) Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na Wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyokatika waraka **Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**

ix) Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mafunzo mbali mbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

x) Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimethibitishwa na Mamlaka husika (**NACTE na NECTA**).

xi) Uwasilishaji wa Taarifa na Sifa za kughushi, wahausika watachukuliwa hatua za kisheria

xii) Barua ya maombi itatakiwa iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.

xiii) Mwisho wa kupokea barua za maombi ni Jumanne, tarehe **26 Machi, 2024**.

xiv) **MUHIMU:** kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, aidha anuani ya barua hiyo elekezwe kwa;

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Handeni,
S.L.P 355,
HANDENI.

xv) Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kielekroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal')

xvi. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**



Yibarila C. Kamele
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HANDENI.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HANDENI